

SHULE YA JUMAPILI YA CBM

Awamu ya 2 Mwaka wa 2



55 Mungu ananena na Samweli

Kwa Biblia

1 Samweli mlango wa 1 na 3

Kiini cha somo

Kuonyesha kwamba Mungu hujibu maombi. Lazima tufunze watoto wetu kuomba Mungu. Lazima tutimize ahadi zetu

Somo

Elkana aliishi na wanawake wake wawili Hana na Penina. Penina alikuwa na watoto gadhaa. Lakini Hana hakukuwa na watoto. Hana alikuwa na huzuni kwa sababu hakukuwa na watoto. Penina alikuwa akicheka Hana kwa hivyo Hana akawa na huzuni zaidi.

Kila mwaka, familia hii walisafiri kwenda Shilo kuabudu Mungu. Walikuwa na karamu huko Shilo wakifurahi na kushukuru Mungu. Elkana aliwapa Penina na watoto wake chakula. Elkana alimpa Hana chakula kizuri zaidi kwa sababu alimpenda sana. Penina alikuwa na wivu kwa Hana. Alicheka Hana kwa sababu Hana hakukuwa na watoto.

Hana hakukuwa na furaha wala hakukula. Elkana alimpa chakula kizuri sana lakini hangekula kwa kutokuwa na furaha. Hana aliamua kuambia Mungu shida zake. Hana alienda kwa nyumba ya Mungu, akapiga magoti na kuomba Mungu. Alizungumza na Mungu kwa muda mrefu.



Maswali

1. Mbona Hana hakukuwa na furaha?
2. Mbona hana hangeweza kukula?
3. Hana alienda wapi?
4. Hana aliuliza Mungu nini?
5. Ahadi gani yenye Hana aliahidi Mungu?
6. Mungu alijibu maombi ya Hana namna gani?
7. Hana aliweka hiyo ahadi kwa Mungu namna gani?
8. Nani aliita Samweli usiku?
9. Mwanzoni Samweli alifikiri nani alikuwa akimuita?
10. Mungu aliambia Samweli nini?

Majibu


1. Hana hakukuwa na mtoto.
2. Hana hangewezakula kwa sababu alikuwa na huzuni.
3. Hana alienda Hekaluni.
4. Hana aliuliza Mungu ampe mwana.
5. Hana aliahidi kumpa Mungu huyo mwana na ataishi kwa Hekalu.
6. Hana alipata mwana mwaka uliofuata.
7. Hana alipeleka Samweli Hekaluni ili asaidia Eli.
8. Mungu aliita Samweli usiku.
9. Mwanzoni Samweli alifikiri Eli ndiye alikuwa akimuita.
10. Eli na wanawe wawili watakufa. Samweli atakuwa nabii mkuu tena kiongozi.

Kuhani Mkuu alikuwa Eli. Eli aliona Hana akiomba. Hana aliomba Mungu kwa muda mrefu. Hana aliambia Mungu shida zake zote. Hana hakuzungumza na Mungu kwa sauti lakini midomo ndiyo ilikuwa ikisema. Eli hakujua kwamba Hana alikuwa na huzuni. Eli alifikiria kwamba Hana alikuwa mlevi. Eli aliudhika sana. Hana alielezea Eli kwamba yeye ana huzuni, kwa hivyo ako anaambia Mungu shida zake. Eli aliposikia hiyo alitabasamu na akamwambia, “Enda kwa amani na Mungu akufanyie vile umemuomba.”

Hana alifurahi baada ya kuomba Mungu. Aliamini kwamba Mungu atajibu maombi yake. Mwaka uliofwata Hana alipata mtoto mvulana. Hana aliita huyo mtoto ‘Samweli’ maana yake, ‘niliomba Mungu.’ Hana alikaa nyumbani na Samweli wakati alikuwa mdogo sana. Hakuenda na familia Shilo kuabudu Mungu.

Hana alikuwa ameahidi Mungu kwamba akizaa mtoto mvulana atampeana kwa Mungu. Hana alijua lazima atimize hiyo ahadi kwa Mungu. Samweli alipokuwa mkubwa Hana alimpeleka Shilo kwa Mungu. Aliambia Eli kwamba Samweli ni mtoto aliyeomba Mungu. Aliambia Eli kwamba aliahidi Mungu eti Samweli atakapokuwa mkubwa atafanya kazi kwa nyumba ya Mungu na kumwabudu milele.

Eli alifurahi kuwa na Samweli akimsaidia kazi. Eli alikuwa mzee. Wana wa Eli walikuwa waovu na wachoyo. Hawakusaidia Eli kufanya kazi. Kwa hivyo alifurahi alipopata Samweli amsaidie.



Samweli alikuwa na furaha sana alipokuwa akisaidia Eli kazi kwa nyumba ya Mungu. Kila mwaka Hana alizuru Shilo kumuona Samweli. Kila baada ya mwaka moja Samweli alikuwa amekua kidogo. Aliletea Samweli nguo mpya za kuvaa. Hana alipata watoto wengine baada ya Samweli. Hao watoto wengine walikaa na Hana Nyumbani.

Usiku moja Samweli aliamka. Alisikia sauti ikimwita, “Samweli, Samweli.”

Samweli alidhani Eli ndiye alikuwa akimwita. Alikimbia kwa Eli akitaka kujua alichomtakia. “Sikukuita,” Eli alimjibu, “Rudi ulale.”

Mara tatu Samweli alisikia hiyo sauti ikimwita. “Samweli, Samweli.” Kila wakati alikimbia kwa Eli. Lakini Eli hakukuwa amemwita. Baadaye Eli alikumbuka kwamba lazima awe Mungu ndiye alikuwa akimwita Samweli. Eli alimwambia, “Ukisikia sauti tena, ujibu, ‘Sema Bwana nimekusikiliza.’”

Samweli alirudi kulala. Aliongoja kwa utulivu. Mungu alimwita tena. “Samweli, Samweli.” Samweli alijibu, “Sema Bwana nimekusikiliza.”

Mungu aliambia Samweli kwamba wana wa Eli ni waovu. Eli hakukuwa akiwaongoza vizuri. Mungu alimwambia kwamba Eli na wana wake wawili wanaenda kufa. Mungu alifurahia Samweli kwa sababu alipenda Mungu na alikuwa anafanya kazi kwa nyumba ya Mungu kwa nguvu. Mungu alisema atafanya Samweli kuwa nabii mkuu. Samweli atafundisha watu wajue Mungu.

Asubuhi iliyofuata Samweli aliamka mapema. Alianza kufanya kazi yake. Eli alimuita na kusema, “Niambia kila kitu chenye Mungu alikwambia. Usiogopa kuniambia.” Samweli aliambia Eli kila kitu chenye Mungu alisema. Eli alijua kwamba wana wake walikuwa waovu. Alisema, “Nimapenzi ya Mungu. Wacha Mungu afanye kilichohaki.”

Samweli alikua akiamini Mungu na kumtii. Alifundisha watu juu ya Mungu. Akaendelea kuwa nabii mkuu na kuwa kiongozi wa Israeli.